

**HOTUBA YA MHESHIMIWA MKUU WA MKOA WA RUKWA  
ZELOTE STEPHEN ZELOTE WAKATI YA UZINDUZI NA  
UGAWAJI WA VITAMBULISHO VYA TAIFA KWA WATUMISHI  
WA UMMA MKOANI RUKWA TAREHE 13 APRILI, 2017**

Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa,

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa,

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,

Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga,

Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya,

Wakuu wa Mashirika ya Umma, Taasisi za Serikali na Idara  
zinazojitegemea,

Watendaji wa Serikali,

Watendaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA),

Waandishi wa Habari,

Wageni Waalikwa,

**Mabibi na Mabwana.**

Kwanza nimshukuru Mungu aliyetujalia kukutana hapa siku ya leo  
tukiwa wenye nguvu na afya tele.

Pia niwashukuru waandaaji wa NIDA kwa heshima ya kunialika kuwa  
mgeni rasmi katika tukio hili kama ishara ya kuanza utoaji wa  
vitambulisho vya Taifa katika Mkoa wa Rukwa.

## **Ndugu Katibu Tawala,**

Napenda kuwapongeza watendaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) waliopo ndani ya Mkoa wa Rukwa kwa kuanza vyema zoezi hili. Ni matumaini yangu kwamba mtafanya kazi hii kwa weledi lakini pia kwa uaminifu wa hali ya juu kutokea dosari ya namna yoyote kupoteza maana na umuhimu wa zoezi hili linaloendelea katika Taifa letu. Nataka nisisitize; mlengwa katika zoezi hili ni Mwananchi wa Tanzania na siyo vinginevyo. Baada ya kuandikishwa kitambulisho rasmi kitatolewa. Ni jukumu la kila mtu kutunza kitambulisho chake na kukionyesha pale kitakapohitajika kwa utambulisho au matumizi mengineyo.

## **Ndugu Katibu Tawala,**

Ningependa kuisitiza kwamba suala la vitambulisho vya Taifa lipo kisheria. Sheria ya uandikishaji na utambuzi wa Raia inapatikana katika Sura namba 36 iliyofanyiwa maboresho Mwaka 2012 (Registration and Identification of Persons Act) Kifungu namba 7 inaeleza kila Raia mwenye umri kuanzia miaka 18 kwenda juu na ambaye anaishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye sheria hii inamtambua inamtaka aombe maombi ya kuandikisha uraia kama sheria hii inavyomtaka.

Kifungu cha 20 kifungu kidogo cha 1(a)-(f) cha sheria hiyo kinaainisha makosa na adhabu kwa mtu yoyote anayekiuka maagizo katika kifungu cha 7. Baadhi ya makosa hayo ni:-

1. Kuharibu kadi ya utambulisho kwa makusudi
2. Kutoa taarifa za uongo kwa msajili
3. Kumzuia kwa makusudi Msajili au Afisa Uhamiaji wakati wa zoezi la kuandikisha

## **Ndugu Katibu Tawala,**

Natambua kwamba zoezi hili la vitambulisho vya Taifa limeanza kwa watumishi wa umma na litaendelea kwa wananchi wote. Wito wangu kwenu Watendaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa mhakikishe mnaweka utaratibu mzuri utakaomwezesha kila Mwananchi kujiandikisha bila usumbufu, ucheleweshaji ama kero ya aina yoyote. Mkumbuke mtakutana na watu wa aina tofauti wakiwepo wazee, vijana, walemavu na waja wazito. Ni jukumu lenu kujipanga namna ya kurahisisha huduma kwao. Toeni ratiba zenu mapema kuwandaa wananchi. Shirikianeni na Watendaji wa Halmashauri ngazi ya Vijiji, Kata n.k.

Ningependa kutoa wito kwa wananchi wajitokeze katika zoezi hili mapema na sio kusubiri siku za mwisho. Katika zoezi hili nitapenda wananchi watoe ushirikiano kwa mamlaka husika.

## **Ndugu Katibu Tawala,**

Kabla ya kuhitimisha maneno yangu kwa leo ningependa kutoa rai kwa wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa kujiandaa kikamilifu kwa zoezi linalokuja la usajili na utambuzi kwa ajili ya kupata vitambulisho vya Taifa. Andaeni viambatanisho muhimu vitakavyosaidia ninyi kutambulika kwa urahisi.

Viambatanisho msingi ni pamoja na vile vinavyohitajika kuthibitisha umri, Makazi na Uraia, kama vile cheti cha kuzaliwa, hati ya kusafiria, Vyeti vya shule, kadi ya kupigia kura, kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, TIN namba n.k. Kuwa na vitambulisho vingi ni kutambulika kwa haraka na kurahisisha uandikishaji.

Nipende pia kuwasihi na kuwaomba viongozi wa dini na siasa kutoa ushirikiano kwa kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na kwa wakati na kujitokeza katika zoezi hili.

Baada ya kusema hayo sasa ninatamka kuwa zoezi la utambuzi, uandikishaji na ugawaji wa Vitambulisho vya Taifa Mkoani Rukwa limezinduliwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Zelote Stephen Zelote  
**MKUU WA MKOA WA RUKWA**